VIDOKEZO KWA WAKULIMA

Imebuniwa Tanzania, Septemba 2013

Mbegu kinzani kudhibiti wa kirusi cha njano kwenye mpunga

Tambua tatizo

Ugonjwa wa kirusi cha njano ni ugonjwa ambao hushambulia zao la mpunga.Mimea iliyoathirika huwa na michirizi ya njano au machungwa kwenye majani hasa katika hatua za awali za ukuaji wa mmea.Mimea iliyoathirika zaidi majani yake hujikunja na kukauka.Dalili nyingine ni kudumaa kwa mimea,machipukizi machache, mashuke hayajazi vizuri na kuwa mapepe na punje hupungua ubora.Upotevu wa mazao unakadiriwa kuwa 25-100%kutegemeana na aina ya mbegu.

Majani yaliyoathirika yakionesha rangi za njano na machungwa. (Picha na Sy & Yacoubav)

Habari tangulizi

Ugonjwa huu huenezwa kwa njia ya palizi na visumbufu ambavyo hufyonza majimaji kutoka mimea ilioathirika na kusambaza kwenye mimea mizima. Visumbufu vinavyoeneza ugonjwa huu ni kama panzi na vidugamba.

Usimamizi

- Tumia mbegu kinzani zilizothibitishwa kama; Mwangaza(SSD35), Lunyuki, Giganta WABIS 844,IRAT 254 na IR47686-15-5.
- Mbegu hizi zinapatikana katika maduka ya mbegu yaliyosajiliwa
- Mbegu hizi huoteshwa na kuhudumiwa kama ilivyo kwenye mbegu nyingine.
- Njia nyingine zinazofaa kutumika katika kudhibiti ugonjwa huu ni;
- Usafi wa shamba na mazingira yanayozunguka ili kuondoa masalia ya ugonjwa kutoka kwenye mabaki ya mpunga wa msimu uliopita na magugu
- Tumia viuatilifu ili kudhibiti visumbufu vya mimea ambavyo vinasambaza ugonjwa hasa kwenye vitalu mfano bidhaa za Fenvalerate kama Fenvil, Kotkil na viuatilifu vingine ambavyo vimependekezwa na daktari wa mimea.Chukua tahadhari katika kutumia bidhaa ambazo zina madhara zaidi,(Soma vibandiko kuhusu matumizi).Vaa mavazi ya kujikinga.Usipulizie sumu kwenye mpunga ambao uko tayari kuvunwa.
- Chukua tahadhari wakati wa palizi kuepusha kusambaa kwa ugonjwa.
- Zingatia mzunguko wa mazao kwa kupanda mazao mengine kama mahindi au mbogamboga ili kuzuia kuenea kwa ugonjwa kwa njia ya wadudu wafyonzao.

Mbawa kavu akifyonza jani la mpunga lenye ugonjwa ambao atausambaza atakapo fyonza jani lingine la mpunga wenye afya. (Picha na gbohne)

Daraja la 1 la viwatilifu kulingana na shirika la Afya Duniani (WHO) (na bidhaa yenye kibandiko chekundu kwaTanzania) hazishauriwi kutumika. Daraja la II la viwatilifu kulingana na WHO (na bidhaa yenye kibandiko cha njano-Tanzania), (hazishauriwi Tanzania kutokana na Mpango wa Udhibiti Husishi wa Visumbufu vya Mimea). WHO hupendelea daraja la 3 au U, na Tanzania inashauri bidhaa zenye kibandiko cha kijani au bluu. Kagua na zingatia kutumia Viwatilifu vilivyosajiliwa na (MAFC / TPRI).

Wakati wa kutumia kemikali, vaa mavazi ya kinga wakati wote na ufuate maelekezo kwenye lebo ya bidhaa, kama vile kipimo, majira ya kuweka, muda kabla ya kuvuna

Jina la kisayansi **> *Rice yellow mottle virus RYMV***

Mapendekezo katika vidokezo hivi yanatumika katika: Tanzania

Ministry of Agriculture, Food Security & Cooperatives
United Republic of Tanzania

WAANDISHI: Edith D. Kija Mariam I. Mziray, Jubilant JN Mwangi
DED, Morogoro District Council, Kiroka, P.O Box 747 Morogoro, Tanzania;
Ministry of Agriculture, Food Security and Cooperatives MAFC, P.O Box 9071
Simu: +255 713992204, +255713234338 Barua pepe: edithkija@yahoo.com, mamziray@yahoo.com

Mwisho na Plantwise.

Plantwise is a global initiative led by CABI

Lose Less, Feed More

©CAB International. Published under a CC-BY-SA 4.0 licence.